**UCHAMBUZI WA MSWAADA WA FEDHA WA MWAKA 2024 ULIO WASILISHWA KWA KAMATI YA BAJETI YA BUNGE MJINI DODOMA TAREHE 23/06/2024**

## 1. 0. Kuhusu Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) ni shirika la uanachama linalojumuisha mashirika ya haki za binadamu Zaidi ya 300 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Ulisajiliwa mwaka 2012 chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002. Lengo kuu la THRDC ni kuchangia ukuaji wa nafasi ya kiraia ambapo mazingira ya kazi za Watetezi wa Haki za Binadamu (HRDs) yanaboreshwa kwa mujibu wa Tamko la Umoja wa Mataifa la mwaka 1998 kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu. THRDC inafanya kazi Tanzania nzima (Bara na Zanzibar) na imegawa wanachama wake katika kanda 11 za utendaji ambazo zimewezesha upatikanaji wa huduma na msaada kwa HRDs waliopo mashinani. Kwa sasa, Muungano una ofisi mbili, makao makuu Dar es Salaam na tawi la THRDC Zanzibar.

THRDC imewekeza kwa muda mrefu katika uimarishaji uwezo wa Watetezi wa haki za binadamu na asasi za kijamii ili kuongeza ufanisi katika kulinda na kukuza haki za binadamu hapa nchini na kuwahudumia watanzania kwa ujumla.. Ni kupitia lengo hili THRDC kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa NGOs, NaCoNGO pamoja na wadau wengine umekuwa ukifanya kazi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa takriban miaka mitano sasa kutatua masuala ya Uzingatiaji wa Kodi kwa AZAKI.

## 1.**1 Kuchambua Mswaada wa Fedha wa 2024**

Sekta ya AZAKI inajukumu muhimu katika kukuza ukuaji wa uchumi, kuendeleza jamii, kuboresha jamii, na kukuza ushiriki wa raia. AZAKI ni muhimu sana kwa maendeleo ya kijamii na uchumi wa nchi ambapo uwezo wa serikali na mapato ni mdogo. Sekta ya AZAKI nchini Tanzania imetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi katika sekta zote za uchumi. Hizi ni pamoja na kusaidia umma katika kupunguza umaskini, mabadiliko ya sera na sheria, ulinzi wa mazingira, utoaji msaada wa kisheira, kulinda haki za binadamu, utoaji wa huduma za msingi, na uimarishaji wa uwezo miongoni mwa AZAKI zingine.

A) **Muhtasari wa Muktadha:** Sehemu ya X ya "Mswaada wa Fedha wa 2024" inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332. Hasa, Kifungu cha 64 kimepangwa kurekebishwa ili kujumuisha uendelezaji wa afya na ulinzi wa mazingira kama vigezo vya kupata hadhi ya shirika la hisani. Lengo la marekebisho haya ni kukuza huduma za hisani

zinazohusiana na afya na ulinzi wa mazingira na kushughulikia athari za mabadiliko ya hali ya hewa duniani.

**B)** Marekebisho yanayopendekezwa yamepanua utambuzi wa shughuli za hisani kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali. Kujumuishwa kwa afya na ulinzi wa mazingira kama vigezo vya hadhi ya hisani kunatambua umuhimu wa sekta hizi. Mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi katika nyanja hizi yatakidhi vigezo vya kutambuliwa kama mashirika ya hisani wakati mashirika mengine yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi katika maeneo mengine kama haki za watoto, ukatili wa kijinsia, watoa msaada wa kisheria, watoa huduma za kijamii, haki za kiuchumi, haki za binadamu kwa ujumla yanaendelea kutozwa kodi kama mashirika ya kibiashara. Tunapongeza sana serikali kwa kuona umuhimu wa kufanya maboresho haya. Hata hivyo tunadhani bado kifungu hiki kinaweza boreshwa na kutaja maeneo mengine yanayanyiwa kazi na AZAKI. Uchambuzi huu umetokana na mapendekezo ya AZAKI yaliyomo katika taarifa yao kuhusu changamoto za kodi kwa sekta ya AZAKI.

## 2.0 Changamoto za Sasa kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

2.1 **Kodi kwa AZAKI:** Mashirika yasiyo ya kiserikali yanatozwa kodi kama taasisi za kibiashara. Yanatozwa kodi ya kampuni kwa 30% ya mapato yanayotokana na ada za wanachama, michango, na misaada. Pia wanalazimishwa na sheria kufanya malipo kila robo mwaka kama makampuni ya biashara kulingana na Kifungu cha 88 cha Sheria ya Kodi ya Mapato (RE 2019). Yanatakiwa kuwasilisha taarifa za mwaka ndani ya miezi sita baada ya mwisho wa mwaka (Kifungu cha 91(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato).

2.2 NPOs zinatakiwa pia na sheria kuwasilisha makadirio ya kodi ya mwaka wakati NPO hupokea tu misaada kutoka kwa wafadhili na michango kutoka kwa wanachama, si mapato. NPOs hazipati mapato wakati wowote, bali vyanzo vyao vya mapato ni michango kutoka kwa wanachama, michango kutoka kwa wapenda maendeleo na misaada kutoka kwa washirika ambayo inaweza kutumika kwa miaka miwili au mitatu. Changamoto hapa ni neno "mapato"; NPOs hazina mapato bali ni misaada na michango tu. Misaada yoyote kutoka CSOs inayovuka kutoka mwaka mmoja kusaidia shughuli za mwaka mwingine siyo mapato wala faida inayotozwa kodi.

2.3 Kutokujumuishwa kwa AZAKI katika Kamati ya maboresho ya kodi iliyoundwa chini ya kifungu cha 11 cha Kanuni za Bajeti, 2015 chini ya kifungu cha 63 cha Sheria ya Bajeti, 2015 (Na: 11 ya 2015).

2.4 **Hadhi ya Hisani;** AZAKI zinaweza kupata hadhi ya hisani kupitia uamuzi wa binafsi wa Kamishna chini ya Kifungu cha 11 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438, ikiwa zitakidhi vigezo chini ya Kifungu cha 64(8) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332. Mchakato huu una urasimu na unachukua muda mrefu. Kwa upande wa Tanzania, AZAKI bado zinachukuliwa kama walipa kodi na zimewekwa katika kundi moja na kampuni za biashara kulipa kodi ya mapato. Mfumo wa kodi nchini Tanzania una masharti yasiyoeleweka ambayo yanahitaji AZAKI kuomba msamaha wa kodi wa sehemu pale wanapohisi wanastahili msamaha wa kodi. Hii ni kusema kuwa AZAKI zote nchini Tanzania ni walipa kodi kama kampuni za biashara hadi hadhi ya msamaha itakapowasilishwa na kupitishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

2.5 **Ufafanuzi wa Sasa wa Mashirika ya Hisani:** Kifungu cha 64(8) kinafafanua mashirika ya hisani kama vyombo vya umma vinavyojikita kwenye kupunguza umaskini, kuendeleza elimu, au utoaji wa afya na miundombinu.

Marekebisho yanayopendekezwa kutoka Mswaada wa Fedha wa 2024 yanajumuisha uendelezaji wa afya na ulinzi wa mazingira kama vigezo vya kupata hadhi ya shirika la hisani. Ingawa tunapongeza maendeleo haya, AZAKI zinazofanya kazi katika maeneo haya bado zinakumbana na kodi isipokuwa wapate hadhi ya hisani na mchakato unabaki kuwa wa urasimu.

Marekebisho haya yanapaswa kupanuliwa kujumuisha maeneo yote yanayofanyiwa kazi na mashirika yasiyo ya faida kama watoa msaada wa kisheria, kukuza na kulinda haki za binadamu, watoa huduma za kijamii, mashirika ya kibinadamu, mashirika ya uwezeshaji wa kiuchumi wa jamii, nk.

2.6 **Sheria haitofautishi kati ya mashirika yanayofanya faida na yasiyo ya faida:** Mfumo wa kodi nchini Tanzania umeweka kundi moja AZAKI na walipa kodi wengine ambao wanafanya faida. Kimsingi, AZAKI si walipa kodi bali ni mawakala wa kodi kwa niaba ya TRA. Kusajili AZAKI kama Kampuni, ni kuzifanya zikidhi mahitaji ya kodi sawa na mashirika yanayofanya faida. Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato, Mashirika Yasiyo ya Kufanya Faida yanachukuliwa kama kampuni. Mashirika Yasiyo ya Kufanya Faida yanahusishwa tu na "Shirika la Hisani" kwa kifungu cha 64(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ambacho siyo cha moja kwa moja kulingana na masharti yaliyowekwa chini ya Kifungu cha 64(8).

## 3.0 Mapendekezo

3.1 .Kuboresha na kupanua zaidi tafsiri ya mashirika ya hisani ili kuendana na sheria za NGOs, kuhakikisha kuwa AZAKI zote zinazofanya kazi kwa manufaa ya umma na kutoa misaada zinastahili misamaha ya kodi. Hivyo, tunapendekeza tafsiri ya Shirika la Hisani kama ifuatavyo:

‘***Shirika la Hisani*** *ni aina ya kikundi cha hiari cha watu binafsi au mashirika kilichosajiliwa kama taasisi na kisichogawana faida ili kufikia malengo yanayowanufaisha umma au sehemu kubwa ya umma kwa kujikita katika kushughulikia ustawi wa jamii ikiwa ni pamoja na kutoa huduma mbalimbali za kijamii, kiuchumi, kielimu, kisheria, kiafya, kiutamaduni, kimazingira, na za kibinadamu, pamoja na kukuza haki za binadamu, utawala bora; uwajibikaji wa kijamii na kutoa msaada wa kisheria kwa umma. Mashirika ya hisani yanatambuliwa kwa kujitolea kwao katika kuomba rasilimali ndani na nje ya nchi au kutumia rasilimali zao na juhudi kuboresha ustawi wa jamii, bila nia ya kugawana faida kwa manufaa ya binafsi.’*

3.2 **Kurahisisha utaratibu wa kupata hadhi ya hisani ili kupunguza urasimu.** Shirika lisilo la faida linakuwa shirika la hisani baada ya kutolewa uamuzi na Kamishna chini ya Kifungu cha 11 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 baada ya kuridhika kuwa, uanzishwaji, malengo na kazi za chombo hicho ni sawa na zinazo fafanuliwa chini ya Kifungu cha 64(8) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332.]

3.3 Kifungu cha 11 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 na Kifungu cha 64(8) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332 inapaswa kurekebishwa ili kuakisi hili. Kuweka mazingira mazuri

ya AZAKI katika sheria za kodi.. Sheria inapaswa pia kutumia maana ya Shirika la Hisani kama ilivyo katika Sheria ya NGOs. vi.

**3.4** Kuepuka adhabu na riba zisizolipika za kodi, tunashauri serikali kufanya mapitio ya Kifungu cha 78 (1) na (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi kwa kufuta sharti la adhabu ya kila mwezi kwa kushindwa kujaza marejesho ya sifuri kwa Mashirika Yasiyo ya Faida ambayo hayajapata misaada.

Marekebisho yanayopendekezwa ya Kifungu cha 64 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ni hatua nzuri kuelekea kusaidia mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojikita kwenye afya na ulinzi wa mazingira. Hata hivyo, ulinganifu zaidi na sheria za NGOs na urahisishaji wa mchakato wa msamaha wa kodi ni muhimu ili kuunga mkono kikamilifu sekta ya mashirika yasiyo ya kiserikali. Kwa kupitisha mapendekezo haya, watunga sera wanaweza kuhakikisha mazingira mazuri kwa mashirika yote ya hisani, kuwawezesha kustawi na kuchangia kwa ufanisi katika ustawi wa jamii na uendelevu.

**4. Hitimisho**

Mswaada wa Fedha wa mwaka 2024 unaleta marekebisho kadhaa kwenye sheria zilizopo za kodi na zisizo za kodi ili kurekebisha sera za kiuchumi na kuboresha sekta mbalimbali, ikiwemo kilimo, viwanda, na utawala wa mitaa. Pendekezo muhimu linawawezesha walipa kodi kuwasilisha nyaraka kwa Kamishna Mkuu kwa njia za kielektroniki, na kufanya rasmi utaratibu uliopo. Zaidi ya hayo, mswaada uliopendekezwa unaleta kodi kwa huduma za kidijitali na mapato ya kodi za pango. Aidha, mswaada unaleta kanuni mpya za shughuli za michezo ya kubahatisha, ikiwa ni pamoja na vyeti vya wauzaji na marekebisho ya adhabu.

Tunapongeza serikali kwa kuhakisha kila mtanzania mwenye kutakiwa kulipa kodi kulingana na kipato chake analipa kodi. Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato (Sehemu ya X) Kifungu cha 3 kinaanzisha kodi kwa huduma za kidijitali na mapato ya kodi za pango wakati Kifungu cha 10 kinaongeza viwango vya kodi kwa watu binafsi na makampuni.

**Mtazamo wa Haki za Binadamu:** Kodi za juu kwa huduma za kidijitali zinaweza kupunguza upatikanaji wa taarifa na haki za kidijitali, hasa kwa watu wenye kipato cha chini. Kuongezeka kwa kodi za mapato ya kodi za pango kunaweza kuathiri uwezo wa kumudu makazi. Wakati tunatambua kila mtanzania anapaswa kulipa kodi kwa kila kipato chake tunapenda kushauri kuwe na umakini mkubwa katika kodi hizi za watumia mitandao ili zisije tumika kubinya uhuru wa kutumia mitandao. Mswaada huu unataka wale watumia mintandao ( soclia influencers ) wakatwe kodi ya zuio kwa asilimia tatu. Hatuna tatizo na kila mwenye kipato kulipa kodi ya mapatao ila tunatoa angalizo kuwa kifungu hiki kisijetumika kubinya uhuru wa kutumia mitandao.

Tunashukuru kamati ya Bunge kwa kupokea mawasiilisho haya na tuna imani tafsiri ya AZAKI. Ya Hisani itaboreshwa kwa kuzingatia mapendekezo haya ya sekta ya AZAKI.

**IMEWASILISHWA NA:**
**Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)**
**23 JUNE 2024**
**DODOMA**